BODI YA KOROSHO TANZANIA



# KALENDA YA TASNIA YA KOROSHO NCHINI

IMETAYARISHWA NA
Mkurugeniz Mkuu,
Bodi ya Korosho Tanzania,
S.L.P 533
Mtwara.

Januari, 2021

# YALIYOMO


SEHEMU YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI

1.1 Umuhimu wa Kalenda katika Tasnia ya Korosho Tanzania....2

SEHEMU YA PILI

2.0 KALENDA TA TASNIA YA KOROSHO TANZANIA

2.1 Kalenda ya Kilimo cha Korosho Tanzania....3

2.2 Kalenda ya Matukio Muhimu katika Tasnia ya Korosho Tanzania....3

SEHEMU YA TATU

3.0 KALENDA YA KILIMO CHA KOROSHO TANZANIA....4

SEHEMU YA NNE

4.0 KALENDA YA MATUKIO MUHIMU KATIKA TASNIA YA KOROSHO TANZANIA....6

SEHEMU YA TANO

5.0 HITIMISHO....9

# SEHEMU YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

Tasnia ya korosho ni mojawapo ya tasnia zinazokua kwa kasi hapa nchini. Ni zao la tatu kwa uzalishaji likitanguliwa na zao la pamba katika nafasi ya pili na zao la miwa katika nafasi ya kwanza. Mnamo mwaka 2017/2018 zao la korosho liliongoza kwa kuliingizia Taifa letu fedha za kigeni kiasi cha Dola za Marekani milioni 585.1 sawa na Shilingi Trilioni 1.3. Takwimu hii ni kwa mujibu wa ripoti ya Benki Kuu ya Tanzania iliyotolewa mwaka 2018.

Aidha, kwa mujibu wa sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012, zao hili ni mhimili kwa kaya zaidi ya 500,000 kutoka mikoa ya Mtwara, Lindi, Ruvuma (Tunduru), Pwani na Tanga. Kutokana na umuhimu wa zao la korosho katika kukuza uchumi na kuhifadhi mazingira, zaidi ya mikoa 13 mipya imeanza kulima zao hili. Mikoa hiyo ni pamoja na Mbeya, Morogoro, Singida, Dodoma, Tabora, Songwe, Iringa, Njombe, Katavi, Kilimanjaro, Shinyanga, Kigoma na Rukwa.

### 1.1 Umuhimu wa Kalenda katika Tasnia ya Korosho Tanzania

Zao la korosho kama yalivyo mazao mengine ya kudumu kila mwaka huitaji huduma mbalimbali muhimu. Mathalani; palizi, upogoleaji, ukarabati wa mikorosho iliyozeeka au isiyo na tija (Top working), usambazaji wa viuatilifu na vifungashio, udhibiti wa magonjwa na wadudu waharibifu, ukusanyaji na uuzaji wa korosho sokoni, utayarishaji na upandaji wa miche ya mikorosho n.k. Hivyo, kutokana na ukweli huu Bodi ya Korosho imeona ipo haja ya kuwa na Kalenda ya Tasnia ya Korosho ili kila mdau aweze kutekeleza kwa wakati majukumu yake. Kwa kufanya hivi zao la korosho litaendelea kutoa mchango mkubwa katika ukuaji wa kipato cha mwananchi mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla. Aidha, faida nyingine za kalenda hii ni pamoja na:-

(i) Kuwawezesha wadau wa korosho kujua mtiririko wa matukio katika tasnia ya korosho hapa nchini.

(ii) Kusaidia kufanya maandalizi ya shughuli husika kwa wakati.

(iii) Kuondoa changamoto ya mwingiliano wa majukumu wakati wa utekelezaji.

(iv) Kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa shughuli mbalimbali.

(v) Kusaidia kufanya maandalizi ya mipango mbalimbali ya kuendeleza zao la korosho nchini.

# SEHEMU YA PILI

## 2.0 KALENDA YA TASNIA YA KOROSHO TANZANIA

Kalenda ya Tasnia ya Korosho hapa nchini imegawanyika katika makundi mawili. Kundi la kwanza ni Kalenda ya Kilimo cha Korosho na kundi la pili ni Kalenda ya Matukio muhimu katika Tasnia ya Korosho.

### 2.1 Kalenda ya Kilimo cha Korosho Tanzania

Kalenda ya Kilimo Korosho imezingatia shughuli na matukio yote katika mfumo wa kilimo cha zao la korosho hapa nchini. Kalenda hii imeainisha shughuli za kilimo cha korosho zinazopaswa kufanywa katika msimu wa kiangazi na zile zinazopaswa kufanywa katika msimu wa mvua. Kipindi cha kiangazi ni kuanzia mwezi Mei hadi Novemba huku kipindi cha masika kikianzia Disemba hadi Aprili.

Kalenda hii imeainisha muda na shughuli muhimu za kilimo zinazopaswa kufanywa na mkulima katika maandalizi ya shamba jipya la korosho, namna ya kuendelea kuhudumia shamba la zamani, uboreshaji wa shamba la zamani ikiwa ni pamoja na uondoaji wa mikorosho isiyozaa na kupanda mikorosho mipya.

### 2.2 Kalenda ya Matukio Muhimu katika Tasnia ya Korosho Tanzania

Kalenda hii imeweka bayana matukio muhimu, muda na wahusika wakuu katika utekelezaji. Hivyo, inatarajia kuondoa changamoto za kutofanyika kwa wakati kwa matukio husika. Mathalani, usambazaji wa viuatilifu na vifungashio ambao mara nyingi umekuwa ukicheleweshwa na kuathiri mwenendo mzima wa uzalishaji na masoko ya korosho. Kupitia kalenda hii na endapo itazingatiwa ipasavyo itaongeza ufanisi katika suala zima la uzalishaji na masoko ya korosho hapa nchini.

# SEHEMU YA TATU

## 3.0 KALENDA YA KILIMO CHA KOROSHO TANZANIA

| TUKIO | MSIMU WA KIANGAZI | | | | | | | MSIMU WA MVUA | | | | | WAHUSIKA WAKUU |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | MEI | JUNI | JULAI | AGOST | SEPT | OKT | NOV | DIS | JAN | FEBR | MACH | APRIL | |
| **UANZISHAJI WA SHAMBA JIPYA** | | | | | | | | | | | | | |
| Uondoaji wa vichaka/ mapori. | | | | | | | | | | | | | Wakulima |
| Upimaji na uandaaji wa mashimo. | | | | | | | | | | | | | Wakulima |
| Uandaaji wa kitalu cha miche ya korosho. | | | | | | | | | | | | | Wazalishaji miche |
| Upandaji wa miche na mbegu. | | | | | | | | | | | | | Wakulima |
| Uandaaji wa vikonyo. | | | | | | | | | | | | | Wazalishaji miche |
| Upandaji wa mazao ya muda katika shamba. | | | | | | | | | | | | | Wakulima |
| Palizi. | | | | | | | | | | | | | Wakulima |
| Uondoaji wa maotea/ matawi yasiyo hitajika. | | | | | | | | | | | | | Wakulima |
| **UTUNZAJI WA SHAMBA LA ZAMANI** | | | | | | | | | | | | | |
| Usafishaji wa shamba. | | | | | | | | | | | | | Wakulima |
| Ukaguzi wa shamba. | | | | | | | | | | | | | Mkulima na Afisa Ugani |
| Udhibiti wa magonjwa na wadudu waharibifu. | | | | | | | | | | | | | Wakulima |
| Uboreshaji wa miti iliyozeeka shambani. | | | | | | | | | | | | | Wakulima |
| Uvunaji wa korosho. | | | | | | | | | | | | | Wakulima |
| Ukaushaji wa korosho. | | | | | | | | | | | | | Wakulima |

# SEHEMU YA TATU

## 3.0 KALENDA YA KILIMO CHA KOROSHO TANZANIA

| TUKIO | MSIMU WA KIANGAZI | | | | | | MSIMU WA MVUA | | | | | | WAHUSIKA WAKUU |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | MEI | JUNI | JULAI | AGOST | SEPT | OKT | NOV | DIS | JAN | FEBR | MACH | APRIL | |
| Upelekaji wa korosho ghalani. | | | | | | | | | | | | | Wakulima |
| **UFUFUAJI WA SHAMBA LA ZAMANI** | | | | | | | | | | | | | |
| Usafishaji wa shamba na udhibiti wa magonjwa na wadudu. | | | | | | | | | | | | | Wakulima |
| Uandaaji wa miche na mbegu. | | | | | | | | | | | | | Wakulima |
| Upandaji wa miche na mbegu katika eneo la shamba lililowazi. | | | | | | | | | | | | | Wakulima |
| **UONDOAJI WA MIKOROSHO ISIYOKUWA NA TIJA SHAMBANI** | | | | | | | | | | | | | |
| Utambuzi wa mikorosho isiyo na tija. | | | | | | | | | | | | | Wakulima |
| Ukataji na usafishaji. | | | | | | | | | | | | | Wakulima |
| **UBEBESHAJI WA MITI ISIYOKUWA NA TIJA SHAMBANI** | | | | | | | | | | | | | |
| Utambuzi wa mikorosho. | | | | | | | | | | | | | Wakulima |
| Ukataji. | | | | | | | | | | | | | Wakulima |
| Uotaji wa mashina mapya. | | | | | | | | | | | | | Wakulima |
| Uandaaji wa vikonyo. | | | | | | | | | | | | | Wakulima |
| Ubebeshaji. | | | | | | | | | | | | | Wakulima |
| Uwekaji wa fito katika mashina yaliyobebeshwa. | | | | | | | | | | | | | Wakulima |

***NB: Miezi iliyowekewa kivuli ndio inayohusika na tukio husika.***

# SEHEMU YA NNE

## 4.0 KALENDA YA MATUKIO MUHIMU KATIKA TASNIA YA KOROSHO TANZANIA

| TUKIO | SEPT | OKT | NOV | DIS | JAN | FEB | MACH | APRIL | MEI | JUNI | JULAI | AGOST | WAHUSIKA WAKUU |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Kongamano la Korosho la Dunia (WCC) | | | | | | | | | | | | | WCC |
| Kongamano la Korosho Africa (ACA) | | | | | | | | | | | | | ACA |
| Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Wadau wa Tasnia ya Korosho. | | | | | | | | | | | | | CBT |
| Mafunzo ya Kilimo Bora cha Korosho. | | | | | | | | | | | | | CBT, TARI |
| Mafunzo ya matumizi sahihi na salama ya viuatilifu | | | | | | | | | | | | | CBT, TARI, TPRI |
| Upatikanaji wa mahitaji ya vifungashio (Magunia) na viuatilifu. | | | | | | | | | | | | | CBT, RS, LGA, UNION |
| Uagizaji wa vifungashio na viuatilifu. | | | | | | | | | | | | | TCDC, CBT |
| Ukaguzi na uhakiki wa ubora wa viuatilifu. | | | | | | | | | | | | | TPRI, CBT |
| Usambazaji wa viuatilifu kwa wakulima. | | | | | | | | | | | | | UNION |
| Usambazaji wa magunia kwa Vyama vya Msingi (AMCOS). | | | | | | | | | | | | | UNION |
| Tathmini ya usambazaji wa pembejeo. | | | | | | | | | | | | | CBT |
| Tathmini ya uzalishaji na masoko ya korosho ghafi. | | | | | | | | | | | | | CBT, WADAU |
| Tathmini ya ubanguaji wa korosho. | | | | | | | | | | | | | CBT, WABANGUAJI |

# SEHEMU YA NNE

## 4.0 KALENDA YA MATUKIO MUHIMU KATIKA TASNIA YA KOROSHO TANZANIA

| TUKIO | SEPT | OKT | NOV | DIS | JAN | FEB | MACH | APRIL | MEI | JUNI | JULAI | AGOST | WAHUSIKA WAKUU |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Uzalishaji na usambazaji wa mbegu bora za korosho. | | | | | | | | | | | | | TARI, LGA |
| Mafunzo ya udhibiti wa ubora wa korosho. | | | | | | | | | | | | | CBT |
| Ukaguzi na usajili wa maghala makuu. | | | | | | | | | | | | | CBT WRRB |
| Ufunguzi wa maghala ya AMCOS. | | | | | | | | | | | | | RS, LGA, AMCOS |
| Usajili wa Waendesha Maghala | | | | | | | | | | | | | WRRB |
| Ufunguzi wa maghala makuu | | | | | | | | | | | | | WRRB |
| Ufunguzi wa msimu wa ununuzi wa korosho. | | | | | | | | | | | | | CBT |
| Minada/ mauzo ya korosho za wakulima. | | | | | | | | | | | | | CBT, TMX UNION |
| Uchaguzi wa wadau waliofanya vizuri katika mwaka husika kwa ajili ya kupokea tuzo/zawadi wakati wa Mkutano Mkuu | | | | | | | | | | | | | CBT, WADAU |
| Uchaguzi wa Wakulima bora wa korosho wa mwaka kwa ajili ya kupokea zawadi wakati wa Maonesho ya Nane Nane. | | | | | | | | | | | | | CBT, RS, LGA |
| Maonesho ya Biashara - Saba Saba. | | | | | | | | | | | | | WADAU |

# SEHEMU YA NNE

## 4.0 KALENDA YA MATUKIO MUHIMU KATIKA TASNIA YA KOROSHO TANZANIA

| TUKIO | SEPT | OKT | NOV | DIS | JAN | FEB | MACH | APRIL | MEI | JUNI | JULAI | AGOST | WAHUSIKA WAKUU |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Maonesho ya Kilimo na Mifugo - Nane Nane. | | | | | | | | | | | | | WADAU |
| Maadhimisho ya siku ya kuhamasisha ulaji wa korosho nchini. | | | | | | | | | | | | | CBT |
| Mikutano Mikuu ya Mwaka ya Union. | | | | | | | | | | | | | TCDC, RS, UNION |
| Taasisi za fedha kutoa mikopo ya fedha kwa wakulima. | | | | | | | | | | | | | MABENKI |
| Maandalizi ya Mwongozo wa Usambazaji na Ugawaji wa Viuatilifu | | | | | | | | | | | | | CBT, TCDC, VYAMA VIKUU |
| Maandalizi ya Mwongozo wa Usimamizi wa Masoko na Udhibiti wa Ubora wa Korosho | | | | | | | | | | | | | CBT, TCDC, TMX NA VYAMA VIKUU |

***NB: Miezi iliyowekewa kivuli ndio inayohusika na tukio husika.***

# SEHEMU YA TANO

## 5.0 HITIMISHO

Kalenda hii imeandaliwa kwa lengo la kujenga uelewa wa pamoja juu ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali katika Tasnia ya Korosho hapa nchini. Hivyo ni matumaini ya Bodi ya Korosho Tanzania kuwa itaongeza chachu katika kukabiliana na changamoto zilizokuwa zikijirudia kutokana na ukosefu wa kalenda hii.

**IMETOLEWA NA:-**
Kaimu Mkurugenzi Mkuu,
Bodi ya Korosho Tanzania,
S. L. P 533,
**MTWARA.**
Barua pepe: info@cashew.go.tz
Simu: +255232333536.

CASHEWNUT BOARD OF TANZANIA

KOROSHO